Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 3, Issue 3

7th Dhul-Qa'dah 1431

15th October, 2010

Yaliyomo

Majina Ya Allaah Na Sifa Zake 1– 3

Damu Asilia za wanawake 4

MAJINA YA ALLAAH (عزّ وجلّ) NA SIFA ZAKE

Mtayarishi: Sheikh Muhammad Ibn Saalih al-'Uthaymeen

Msingi Wa Kwanza: Yaliyo Wajibu Kutoka Katika *Maandiko* Ya Qur'an Na Sunnah Kuhusiana Na Majina Ya Allaah Na Sifa Zake.

Kuhusiana na maandiko ya Qur'an na Sunnah ni wajibu (kuhusiana na majina ya Allaah na sifa zake) kuziwacha dalili na maana zake juu ya maana yake halisi bila ya kuzibadilisha. Hii ni kwa sababu Allaah (عز وجلّ) aliiteremsha Qur'an kwa lugha fasaha ya kiarabu na Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiizungumza lugha hiyo ya kiarabu. Kwahivyo, ni waajib kuziwacha maana za maneno ya Allaah (عز وجلّ) na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) kwa vile zote hizo zilikuwa ni kwa lugha ya kiarabu. Vilevile, kuibadilisha hiyo kutoka katika maana yake ya asili itakuwa ni kuzungumza kumuhusu Allaah (عز وجلّ) bila ya ujuzi na jambo hilo limekatazwa kutokana na maneno ya Allaah: **"Sema hapana shaka ameharamisha Mola wangu machafu yote yaliyodhahiri na yaliyofichika (yaliyo fanywa kwa siri) ma'asi, kudhulumu watu pasi na haki, na kumshirikisha Allaah kwa jambo ambalo hakuliteremshia dalili yoyote. Na kumzulia Allaah mambo msiyoyajua."** [al-A'raaf 7:33].

Mfano wa msingi huu unapatikana kwenye maneno ya Allaah (عز وجلّ): **"Bali mikono yake miwili ni yenye kukunjuliwa."** [al-Maa'idah 5:64]. Kwa hakika, jambo lenye kudhihirika kwenye Aya hii ni kwamba Allaah anayo mikono miwili kihakika. Kwahiyo, kuyathibitisha hayo ni waajib, kutokana na msingi huu. Kwahivyo, iwapo mtu atasema yakwamba maana ya mikono yote miwili ni "uwezo", basi ni lazima tumwambie yakwamba huku ni kulibadilisha neno kutoka kwenye asili yake halisi. Na kusema hivyo, hairuhusiwi, kwani ni kuzungumza kumuhusu Allaah (عز وجلّ) pasi na ujuzi.

Msingi Wa Pili: Kuhusiana na Majina Ya Allaah

Kuna vigawanyo vyingi katika msingi huu:

Kigawanyo Cha Kwanza: Majina yote ya Allaah (عز وجلّ) ni mazuri. Maana yake ni kwamba (majina) yote hayo yamemiliki upeo wa juu kabisa wa uzuri. Hii ni kwa sababu kunapatikana ndani yake sifa zenye ukamilifu. Hakupatikani upungufu wowote ndani yake kwa njia yoyote iwayo. Amesema Allaah: **"Allaah, hapana apasae kuabudiwa kwa haki ila Yeye, ana majina mazuri."** [Twaa-haa 20:8]

Mfano wa haya ni jina *ar-Rahmaan,* ambalo ni jina la Allaah (عز وجلّ), kwani linadhihirisha sifa tukufu kabisa, ambayo ni Rehma (Yake) isiyo na kifani.

Tunajua yakwamba *ad-Dahr* (zama) si katika majina ya Allaah (عز وجلّ), kwani halikumiliki upeo wa juu kabisa wa uzuri. Ama kuhusu matamshi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Usizilaani zama, kwani kwa hakika Allaah ni ad-Dahr."* Basi maana yake ni kwamba Yeye ndiye "Msimamizi Mwenye kuzipeleka zama". Mabadiliko haya hutokea kutoka kwenye dalili ipatikanayo kwenye maneno yake (صلى الله عليه وسلم) katika riwaya ya pili (ya hadeeth hii) ambapo Allaah aliposema: *"Kwenye mkono wangu ni amri, naugeuza (kwa mzunguko) usiku na mchana."*

Kigawanyo Cha Pili: Majina ya Allaah hayakufungiwa ndani ya mipaka na idadi maalum.

Haya yametokana na hadeeth mashuhuri: *"Nakuomba, Yaa Allaah, kwa majina yako yote, ambayo uliyojiita kwayo au uliyoyateremsha kwenye Kitaab chako. Au (yale ambayo) uliyomfundisha mmojawapo wa viumbe Vyako, au ambayo uliyoyahifadhi Wewe mwenyewe (na kujihusisha kuyajua) katika 'ilmu iliyofichika (Ghayb) kwako."*

Kutaja na kuyashika kila ambayo Allaah aliyojihifadhia Mwenyewe katika 'ilmu iliyofichikana (*Ghayb*) iliyo kwake, ni vigumu kupatikana. Katika kuunganisha baina ya hadeeth hii na hadeeth nyengine iliyo swaheeh isemayo: *"Kwa hakika, Allaah ana majina tisaini na tisa ambayo (kwayo) mwenye kuyadhibiti (yaani; atakaeyajua kwa moyo, akayasoma na akaomba kwa kuyatumia), basi ataingia Peponi."* ni kwamba maana ya hadeeth hii ni: *"Kwa hakika, miongoni mwa majina (yote) ya Allaah ni majina tisaini na tisa, ambayo kwayo ikiwa mtu atayadhibiti, ataingia Peponi."*

Hii haimaanishi yakwamba majina ya Allaah yamewekewa mpaka wa idadi hiyo (ya 99). Mithili yake itakuwa ni

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

MAJINA YA ALLAAH (عزّ وجلّ) NA SIFA ZAKE

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

iwapo mtu atasema: "Mimi nina dola (pesa) mia moja ambayo nimeshaihesabu kwa malengo ya kuitoa kwa njia ya swadaka." Ukweli huu haukanushi yakwamba yeye anazo dola (pesa) zaidi, ambazo ashaziweka tayari kwa malengo mengine mbali na swadaka.

Kigawanyo Cha Tatu: Majina ya Allaah (عز وجلّ) hayawezi kuthibitishwa kwa kutumia akili, bali huthibitishwa kwa njia ya wahyi (ufunuo ulioteremshwa kutoka kwa Allaah) peke yake. Majina ya Allaah (عز وجلّ) yametegemezwa juu ya ufunuo na kwahivyo, kuthubutu kwake hutegemea yaliyonukuliwa kwenye maandiko yaliyofunuliwa kuhusiana nayo. Kwahivyo, hapana kiwezacho kuongezwa wala kupunguzwa. Hii ni kwa sababu akili yenyewe haina uwezo wa kuyakinisha ni majina gani yenye kumstahiki Allaah. Kwahivyo, ni wajibu kutegemea wahyi (maandiko yaliyofunuliwa) katika kuyabainisha hayo. Vilevile, kumwita Allaah kwa majina ambayo Yeye mwenyewe hakujiita kwayo, au kukataa majina aliyojiita kwayo Yeye mwenyewe, ni hatia dhidi Yake na kumkosea katika haki Yake. Kwahiyo, kujisalimisha kwa taratibu za itifaki kuhusiana na hayo, ni waajib.

Kigawanyo Cha Nne: Maana ya kila mojawapo ya majina ya Allaah yanahusiana na:

1. Allaah Mwenyewe.
2. Sifa yenye kulihusu jina hilo, na
3. Athari ya sifa kama hiyo, iwapo itakuwa ni sifa elekezi.

Kuyaamini majina ya Allaah hakuwezi kukamilika bila ya kuyathibitisha haya yote.

Mfano wa majina hayo ambayo yasiyo elekevu ni jina *al-'Adheem*. Imani ya mtu haikamiliki mpaka aamini yakwamba ni jina la Allaah ambalo maana yake inamuhusu Yeye mwenyewe Allaah, na vilevile sifa yenye kujumuishwa pamoja nalo, ambayo ni Utukufu Wake.

Mfano wa jina elekevu, ni jina *ar-'Rahmaan* (Mwingi wa Rehma). Imani ya mtu haikamiliki mpaka aamini yakwamba ni jina la Allaah linalohusu au kumuhusu:

1. Yeye Mwenyewe Allaah.
2. Sifa yenye kujumuisha, ambayo ni Rehma Zake, na
3. Matokeo yake ambayo ni kwamba Yeye humpa rehma amtakae.

Msingi Wa Tatu: Kuhusiana na Sifa Za Allaah

Vilevile kuna vigawanyo husika katika msingi huu:

Kigawanyo Cha Kwanza: Sifa zote za Allaah ni za daraja ya juu kabisa za ukamilifu na uwezekano wa kusifika. Hapana upungufu upatikanao ndani yake katika hali yoyote iwayo. Baadhi ya mifano ya sifa hizi ni: Kuishi (Kwake), 'Ilmu, Uwezo, Usikivu (kusikiya), Uoni (kutazama), Hikima, Rehma, Utukufu na mengine yasiyokuwa hayo. Hii imetokana na maneno Yake: **"Na ni wa Allaah mfano Mtukufu."** [an-Nahl 16:60]

Sababu pia ni kwamba Allaah ana ukamilifu usiokuwa na shaka, kwahiyo sifa zake ni lazima ziwe zimekamilika. Ikiwa sifa ina upungufu na ina kasoro, basi inazuiwa kutoka Kwake, kwa mfano kifo, ujinga, ukongwe, uziwi, upofu na mengine yasiyokuwa hayo. Hii ni kwa sababu Allaah (عز وجلّ) atawaadhibu wale wenye kumsifu Yeye na sifa za upungufu haliyakuwa Yeye ameepukana na kila upungufu wanaomnasibisha nao Yeye. Pia ni jambo lisilowezekana kwa Mola kuwa na kasoro kutokana na kutoingiliana kwa upungufu, na hali ya Uola.

Ikiwa sifa imekamilika kwa njia moja na upungufu kwa njia nyengine, haitothibitishwa kwa Allaah (عز وجلّ), wala haitozuiwa kutoka kwake katika hali ya kumpwekesha. Bali, tofauti baina ya hali mbili hizo ni lazima ibainishwe. Kwahiyo, itathibitishwa kwa Allaah (عز وجلّ) katika hali ambayo itakapokuwa na ukamilifu na haitowezekana kumthibitishia Yeye kwenye hali ya upungufu. Mifano ya hili ni hila (*makr*), vitimbi (*kaid*), kuhadaa (*khadaa'*) na kadhaalika. Sifa hizi tatu huwa zimekamilika zinapotumika katika kupambana na yenye kufanana nayo (yanapofanywa na mpinzaani) kwa sababu yanaashiriya yakwamba Mwenye kuyafanya hayo, hashindwi kupambana na maadui Zake kwa kitendo chake kama hicho. Na kitakuwa ni upungufu katika hali yoyote nyengine. Kwahivyo, kitakuwa ni chenye kuthibitishwa kwa Allaah katika hali ya kwanza na wala si katika hali ya pili. Amesema Allaah (عز وجلّ): **"Na wanafanya hila. Na Allaah anazipindua hila zao; na Allaah ni m'bora wa kuzipindua hila."** [al-Anfaal 8:30]

"Hapana shaka wao (makafiri) wafanya hila (kwa kutaka kuizima Nuru ya Allaah, Uislamu). Na mimi nitawapulizia na kuwapatiliza mpatilizo (kwa hila zao). [at-Twaariq 86:15-16].

"Hapana shaka wanafiki humdanganya Allaah na Yeye (Allaah) atawalipa kwa kitendo chao (cha kinafiki)." [an-Nisaa' 142]

Kwahivyo iwapo, kwa mfano itasemwa: 'Jee Allaah amewahi kujisifu kwa sifa ya kudanganya Yeye Mwenyewe?" Basi musiseme ndio wala musiseme laa. Badala yake semeni: "Yeye hufanya mipango dhidi ya wale wenye kuyastahiki hayo." Na Allaah ndiye mjuzi zaidi.

Kigawanyo Cha Pili: Sifa za Allaah zinaweza kugawanyika kwenye mafungu mawili: Ambazo zilizothubutu (*Thubootiyyah*) na ambazo zilizokanushwa (*Salbiyyah*).

Thubootiyyah: Kunapatikana ndani yake sifa ambazo Allaah (عز وجلّ) alizojithibitishia Yeye mwenyewe, kama maisha, 'Ilmu na Uwezo.

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

MAJINA YA ALLAAH (عزّ وجلّ) NA SIFA ZAKE

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Kumthibitishia Allaah hizi kwa njia inayomstahiki Yeye ni waajib. Hii ni kwa sababu Allaah (عز وجلّ) amejithibitishia hizo Yeye mwenyewe na Yeye ndiye mjuzi zaidi kuhusiana na Sifa zake.

Salbiyyah: Kunapatikana ndani yake sifa ambazo Allaah alizojikanushia Yeye mwenyewe, kama kudhulumu. Kumkanushia Allaah (عز وجلّ) sifa hizi ni waajib kwa sababu Allaah amejikanushia hizo Yeye mwenyewe. Hatahivyo, ni waajib kuamini katika kuthibitisha kinyume cha ukamilifu wake kwa Allaah, kwani ukanushaji haukamiliki mpaka kupatikane ndani yake kuthibitisha. Mfano wa haya ni maneno ya Allaah: **"Na wala Mola wako hamdhulumu yeyote"** [al-Kahf 18: 49].

Kwahiyo, ni waajib kukanusha sifa ya kudhulmu kutoka kwa Allaah, haliyakuwa kuthibitisha (kinyume chake) sifa ya uadilifu Kwake, kwa njia inayostahiki kabisa.

Kigawanyo Cha Tatu: Sifa zilizothibitishwa (*Thubootiyyah*) zinaweza kugawanyika zaidi kwenye mafungu mawili.

Dhaatiyyah: (Sifa za Dhati Yake): Nazo ni sifa ambazo zisizowacha na wala hazitowacha milele kueleza jinsi Yake, kama vile kusikiya na kuona.

Fi'liyyah: (Sifa za Vitendo Vyake): Nazo ni sifa ambazo zilizoungana na Matakwa Yake (*Mashee-ah*). Yeye akitaka, atafanya, na akitaka, hatofanya, kama vile "Kupanda juu ya 'Arsh" na "Kuja" (Kwake) kama ilivyotajwa kwenye Qur'an: **"Komekani! Wakati itakapo vunjwa vunjwa ardhi. Na akaja Mola wako, na Malaika wamepangana katika swafu. Na ukaletwa siku hiyo moto wa Jahannam."** [al-Fajr 89:21-23]

Yawezekana yakwamba sifa inaweza kuwa ni *Dhaatiyyah* na *Fi'liyyah*, kulingana na kila mojawapo ya sifa mbili, kama vile Matamshi. Kuhusiana na asili ya Sifa, inakuwa ni sifa ya Dhati Yake (*dhaatiyyah*) kwa sababu Allaah (عز وجلّ) hakusimama na wala hatosimama kuzungumza. Na kuhusu kiwango cha mazungumzo yaliyowahi kutoka, ni sifa ya kitendo (*Fi'liyyah*) , kwani matamshi yameungana na Matakwa Yake. Yeye husema Atakavyo, pindi Atakapo.

Kigawanyo Cha Nne: Sifa ya Allaah (عز وج) huleta masuali matatu kwenye akili.

Suali la kwanza: Ni kweli na Ni kwanini?

Suali la Pili: Inaruhusiwa kusema inakuwaje na kwanini?

Sulai la Tatu: Inafaa kufananisha na Sifa za viumbe na ni kwa nini?

Jawabu la kwanza: Naam, ndio, ni kweli. Kwa sababu msingi wenye kuongoza matamshi wenyewe, ni kwamba maana yake ni kweli (sio ishara). Hili halitoweza kutupiliwa mbali, isipokuwa kupatikane dalili iliyo swaheeh yenye kuikataza.

Jawabu la Pili: Laa, hairuhusiwi kuieleza jinsi ilivyo, kutokana na maneno ya Allaah (عز وجلّ): **"Na wala wao (waja) hawaijui 'ilmu Yake Allaah kabisa."** [twa-Haa 20:110]

Vilevile akili haziwezi kufahamu umbile la jinsi zilivyo Sifa za Allaah.

Jawabu la Tatu: Haiwezi kufananishwa na sifa za viumbe, kutokana na maneno ya Allaah (عز وجلّ): **"Hana (Allaah) mfano wa kitu chochote."** [ash-Shuura 42:11]

Na pia, Allaah anastahiki thamani ya upeo wa ukamilifu, kwahivyo, haiwezekani Kwake Yeye kufananishwa na viumbe vyake, kwani hilo ni jambo lenye kasoro na upungufu. Tafauti baina ya *takyeef* (kusema "ni vipi") na *tamtheel* (kusema ni "kama" kadhaa na kadhaa) ni kwamba *tamtheel* ni kuieleza ilivyo jinsi ya sifa kwa kuifungamanisha na mfano fulani, haliyakuwa *takyeef* ni kuieleza ilivyo jinsi ya sifa bila ya kuifungamanisha na mfano fulani.

Mfano wa *Tamtheel*: Ikiwa mtu atasema yakwamba Mkono wa Allaah (عز وجلّ) ni kama mkono wa mwana-adamu.

Mfano wa Takyeef: Ni kuwaza yakuwa Mkono wa Allaah una Umbile aina fulani, usiofanana na chenye kuhusiana na mikono ya viumbe. Aina hii ya mawazo hairuhusiwi.

Msingi Wa Nne: Kiwezacho Kutumika Katika Kuwakosoa Wenye Kufanya *Ta'tweel* (Kukanusha).

Mu'attwilah (wenye kufanya ta'tweel) ni wale wenye kukanusha kila kitu katika majina na Sifa za Allaah (عز وجلّ) na kuzipotosha *nass* kutokana na maana zake halisi. Vilevile wanajulikana kama watu wenye kufanya ta'weel. Nguzo ya msingi ambayo kwayo twaweza kuwakosoa nayo ni kusema yakwamba matamshi yao:

1. Yanakwenda kinyume na uwazi uliobainishwa wa nass;
2. Yanakhalifu ufahamu waliokuwa nao Salaf (watu wema waliotutangulia).
3. Hayana dalili yoyote iliyo swaheeh (ya kuwaunga wao mkono).

Kwa baadhi ya Sifa, huwenda ukawepo mtazamo wa nne, au hata zaidi ya hayo.

NUKTA MUHIMU:

Neno ta'weel linaweza kumaanisha tafsiri au ufafanuzi. Linapotumiwa kumaanisha ufafanuzi, basi litahusu jambo lenye kuruhusiwa, kama vile kufafanua maana ya maneno ya Allaah ni "Juu ya 'Arsh" maana yake ni kwamba Yeye yuko juu kabisa ya viumbe vyote, yakwamba hakuna kiwezacho kumgubika Yeye, na kwamba viumbe vyote viko chini Yake (na kadhaalika). Linapotumiwa kumaanisha tafsiri, basi litahusu jambo ambalo haliruhusiwi, kama kusema yakwamba maana ya "Juu ya mbingu" inahusu upeo wa Utukufu wake na wala haihusiani na Kuwepo kwake Juu ya Mbingu. Katika hali ya pili, tafsiri humalizikia na kukanusha jambo ambalo lililo thibitishwa na *nass* nyengine.

Usikose toleo letu la wiki ijayo

"NASEEHA KWA WENYE NIA YA KWENDA HAJJ"

Endelea Kutoka Vol 3, Issue 2 **... Damu Asilia Za Kina Mama [Sheikh Muhammad bin Swaleh al-'Uthaymeen (رحمه الله)**

Kama mfano wa hayo. Mwanamke ambae kwa mara ya kwanza ameiona damu iliyokuwa ikiendelea kumsibu kuwa ni ya rangi nyeusi kwa muda wa siku kumi na siku zilizobaki za mwezi kuwa ni ya rangi nyekundu. Au aliiona damu kuwa ni nzito kwa muda wa siku kumi na ikawa nyembamba kwa siku zilizobaki za mwezi; au ilikuwa ikitoa harufu ya heidh kwa siku kumi za kwanza na siku zilizobaki za mwezi kutokuwa na harufu. Hapo, ada yake ya mwezi itaweza kuzingatiwa pindi damu itakapokuwa ni nyeusi katika mfano wa kwanza, na pindi damu itakapokuwa ni nzito katika mfano wa pili, na ile damu itakayokuwa na harufu katika mfano wa tatu. Hali zitakapokuwa ni kinyume cha hivyo zitazingatiwa kuwa ni Istihaadhah.

Uamuzi huu umeamuliwa kulingana na hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipomwambia Faatimah Bint Abu Hubaish (رضي الله عنهما) : "Damu ya heidh inatambulika kuwa nyeusi, kwahivyo iwapo itakuwa ni hivyo, usiendelee kuswali. Lakini iwapo damu ilikuwa ni ya aina nyengine tafauti, basi katawadhe na uswali kwa vile ilikuwa ni damu itokayo kwenye mshipa ('Irq)."

Hali Ya Tatu: Ikiwa mwanamke hakuthubutu kuwa na ada ya kila mwezi ya heidh wala hako katika hali ya kuweza kutambua muda wa ada yake ya heidh kisawasawa kwa jinsi damu yake ya Istihaadhah inavyotoka mfululizo tangu alipoanza kuiona damu. Damu inatoka kwa kuendelea ikiwa na sifa zilezile au inatoka kwa sifa za kutatanisha zinazosababisha ugumu katika kupambanua baina ya damu ya heidh kutokamana na ile damu ya Istihaadhah. Katika hali hii, wanawake wanaopata huu urefushaji na mtiririko ambao hawakuutegemea na wazingatie muda wa heidh yao kuwa ni muda unaokabiliwa na wanawake wengi: siku 6-7 za kutiririkwa na heidh kila mwezi, kuanzia wakati atakapo kuiona damu yenye kumwagika. Mbali na muda huu, damu itokayo na izingatiwe kuwa ni Istihaadhaah.
Mfano wa hali hii, ni mwanamke aliyeona ndamu yake kwa mara ya kwanza katika siku ya tano ya mwezi na ikaendelea kutoka nae akawa hawezi kutambua tafauti yoyote katika rangi, harufu wala uzito wa damu. Muda wake wa heidh utakuwa ni siku sita au saba kuanzia siku ya tano ya kila mwezi. Hii ni kulingana na hadeeth ya Hamnah Bint Jahsh (رضي الله عنهما) yakwamba alisema: "Ewe Mjumbe wa Allaah! Mimi nina damu ya Istihaadhah ambayo ni kubwa sana tena yenye nguvu mpaka ikawa ni yenye kunizuiya kuswali na kufunga." Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم) "Nakuusiya utumie Al-Kursuf kwa sababu inanyonya na kuondoa damu." Akasema Hamnah, "Hiyo damu ni nyingi zaidi ya hayo niliyoyasema," Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: "Hilo ni pigo la Shaytaan, kwahivyo mwishoe ada yako itakuwa ni siku sita au saba ambazo zitakuwa katika 'Ilmu ya Allaah. Baada ya kumalizika siku hizo, nenda ukajitwahirishe. Utakapo ona yakwamba sasa umetwahirika, anza kuswali kwa masiku 23 au 24 (usiku na mchana) na ufunge masiku kama hayo."

Maneno yake Mtume (صلى الله عليه وسلم) "ada yako itakuwa ni siku sita au saba" haikumaanisha kumpa Hamnah Bint Jahsh chaguo, bali ni kwake yeye achunguze na aone ni nani (miongoni mwa wanawake wengine) anaemkurubia yeye kwa umri, maumbile ya kimwili, idadi ya watoto, na kadhaalika. Mwanamke atakaeshabihiyana na hali yake anakuwa na muda wa siku sita za heidh, kisha na auzingatie muda huu kuwa ni marejeo yake. Hivyo ndivyo itakavyokuwa iwapo muda wa heidh utakuwa ni siku saba.

Mwanamke Aliye Katika Hali Inayofanana Na Mustahaadhah.

Kuna uwezekano yakwamba tukio fulani (k.m Upasuaji) linaweza kusababisha damu kutoka kwa kupitia kwenye tupu ya mwanamke. Kuna aina mbili za hali hii:

1.**Haiwezekani kwake kupata heidh baada ya upasuaji**.
k.m (kwa mfano) kuondolewa fuko la uzazi au hali ya kulizuiya. Chini ya hali hii, hukmu ya Istihaadhah haiwezi kutumika. Ikiwa mwanamke ataona damu, basi hukmu zinazodhibiti chepechepe ya manjano zitatumika. Kuanzia hapo, asijiepushe na kuswali wala kufunga. Si haraam kwa mumewe kuingiliana nae kimapenzi na wala si waajib juu yake kuoga. Lakini, ni lazima aoge, ajisafishe, na atawadhe katika wakati wa kuanzia swala ya faradhi na anapoazimia kuswali swala ya nawaafil.

2. **Hakuna yakini yakwamba heidh yake itasimama baada ya kufanya upasuaji.**
Inawezekana kwake kupata heidh. Katika hali hii, hukmu zinazompasa Mustahaadhah (mwanamke anaepitia Istihaadhah) pia zitampasa juu ya hali hii kulingana na hadeeth ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipomwambia Faatimah Bint Abee Hubaish: "Hakika damu hiyo inatoka kwenye mshipa ('Irq), na wala si heidh. Kwahivyo ikiwa heidh ya kikweli ikianza, wacha kuswali na itakapomalizika (ada yako) jisafishe damu kutoka mwilini mwako (oga mwili mzima) na uswali."

[Endelea Katika Makala Yajayo]

P. O. Box 85477,
Mombasa,
Kenya.

E-mail: info@qssea.net

QSS (E.A)

جمعية القرآن والسنة في شرق إفرقيا

Tuko katika Tovuti
http://www.qssea.net